



COVID-19


NOVEL CORONAVIRUS



**Kuvaa maski ni muhimu katika kuzuia kuenea kwa COVID-19.
Vaa maski wakati wowote ukiwa kwenye sehemu ya ndani katika
eneo la umma, au wakati ni vigumu kutokaribiana.**

COVID-19 huenea kupyitia kufikiwa na matone ya mate ya mtu aliyeambukizwa. Matone ya Mate yanaweza kuenea kupyitia kupiga chafya, kikohozi, kuimba au kuzungumza. Unaweza kupunguza kuenea kwa matone ya mate yako kwa kuvaa maski inavyofaa.

Jinsi ya kuvaa maski:




1. Nawa mikono yako kwa sekunde 15.



2. Maski ifunike pua na mdomo wako. Mikanda ya maski inapaswa kushikiliwa na masikio yako.



3. Hakikisha maski inafunika pua na mdomo wako.




4. Nawa mikono yako tena kwa sekunde 15.




5. Usijaribu kugusa maski yako wakati umeivaa. Ukiigusa, nawa mikono yako tena.



6. Ukimaliza kutumia maski, vua kwa kutumia mikanda yake.



7. Weka maski chafu kwenye begi ili uisafishe baadaye. Ikiwa ni maski ya kutumiwa mara moja, itupe.



8. Badilisha maski yako ikiwa ni chafu, ina unyevunyevu au imeharibika.